

UZALISHAJI WA NG'OMBE WA NYAMA KIBIASHARA

Apil 2019 By IBRAHIM



UZALISHAJI WA NG'OMBE WA NYAMA KIBIASHARA

UZALISHAJI WA NG'OMBE WA NYAMA KIBIASHARA (Intensive Beef Production) : Mfumo wa sasa wa uzalishaji wa nyamaunahusisha uzalishaji wa mifugo ya nyama tangu ndama hadi kufikia kuuzwa. Utaratibu huu ni wa gharama kubwa sana, kwani unahusisha kutimiza mahitaji ya utibabu, lishe na kuzuia athari zingine (risk) kama wizi kwa muda mrefu wa katii ya miaka 3 – 4 ya ufugaji hadi kufikia umri na uzito wa kuchinjwa.

Mifugo hii hutembea umbali mrefu kutafuta malisho na maji na kuifanya nyama yake kuwa ngumu isiyokidhi ubora unaoitajikwa kwenye soko maalum kama supermarkets,hoteli,

Ileweke kwamba uzalishaji wa nyama huhesabiwa kwa kilo za nyama kwa hekta na si idadi ya ng'ombe. Hivyo basi hatuna budi kuzalisha mifugo kwa utaratibu utakaowezesha ng'ombe kujenga misuli vizuri ili kuzalisha nyama nyingi na bora kwa hekta. Uzalishaji wa mifugo bora ya nyama unahitaji kuzingatia aina ya mifugo (ukoosaafu), malisho bora na kinga dhidi ya magonjwa. Inawezekana kupata uzito wa kuchinja kwa muda mfupi kwa kutumia mfumo wa unenepeshaji mifugo ya nyama. Kuandaa mifugo vizuri toka ikiwa ndama, kuwakuza kwa malisho ya kutosha na baadae kuinenepesha kwa kutumia chakula chenye mchanganyiko wa molasses, bagasse na urea kama inavyoilezwa katika Jedwali (1&2) hapo chini.

Jedwali 1: Kunenepesha Ng'ombe kwa Kutumia Molasses, Majani, Urea na Virutubisho (Preston na Wills (1970) toka Cuba)

Siku	Majani mabichi kg/mnyama	Molasses/urea a,b kg/mnyama	Chanzo cha Protini c g/100kg uzito	Madini d
1	Atakavyo bila kipimo	1.0	120	Atakavyo bila kipimo
2	"	1.5	"	"
3	"	Ongenza 0.5kg / siku hadi siku ya 14	"	"
3 - 14	"	"	"	"
14	"	Atakavyo bila kupimiwa	"	"
15	30	"	"	"
16	25	"	"	"
17	20	"	"	"
18	15	"	"	"
19	10	"	"	"
20 hadi kuchinjwa	1.5kg /100kg uzito	"	"	"

Chanzo: T.R Preston na M.B Willis (1970)

JEDWALI LA KUNENEPESHA NG'OMBE

- a. 2% Urea, 4% Maji, 0.5% Chumvi na 93.5% Molasses
- b. Maji yawe kiwango hicho hicho hadi wiki nne za kwanza zitimie
- c. Unga wa samaki / dagaa (65% protini) au aina yoyote ile ya chanzo cha protini. Mradi ziwe pia 80000 IU za vitamini na 20000 IU za vitamin D kwa kila kilo. Hapa Tanzania vyanzo vya protini vya gharama nafuu ni mashudu ya pamba, alizeti n.k
- d. Madini yenye g/kg; 500 CaHPO₄, 400NaCl, 20 ZnCo₃, 0.1 KI, 19.8, mahindi yaliyopondwa, 27 FeSO₄, 5H₂O, 23MnSO₄, H₂O, 10CuSO₄, 5H₂O, 0.1 CuSO₄, 7H₂O. Hapa Tanzania tumia madini ya Farmer's Superlick na Vitalick toka Farmer's Centre Ltd.

Jedwali 2: Kunenepesha Ng'ombe kwa Kutumia Molasses bagasse na urea na M.E Ruiz (1974) toka Costa Rica.

Siku	Majani Mabichi (a)	Bagasse DM (b)	Molasses	Urea (c)	Meat Bone Meal
	Kg/100kgU*/siku	g/100kgU/siku	Kg/100kgU/siku	g/100kgU/siku	g/100kgU/siku
1-3	5.0	0	0.3	15	50
4-6	2.5	100	0.6	30	100
7-9	1.0	200	1.2	45	200
10-12	0.5	300	2.4	60	300
13 hadi kuchinjwa	0.5	400	2.4	75c	341

U* = Uzito

Chanzo: M.E Ruiz (1974)

KUNENEPESHA NG'OMBE

- a. Huwa yenye 26% DM
- b. Huwa yenye 75% DM
- c. Ifikapo kiwango hiki wanyama wanaweza kutokula, ikitokea hivyo uongezwaji uwe katika viwango vya 60-65-70-75 kila baada ya siku tatu.

HALI YA MINOFU

Minofu inayozalishwa na ng'ombe wa asili ni michache na haikidhi mahitaji ya soko. Ng'ombe wa aina ya Zebu ni wadogo na hukua kwa kasi ndogo, hivyo kuchukua muda mrefu kufikia kuchinjwa na huzalisha minofu kidogo. Kwa mfano nyama ya ng'ombe wa asili iliyokatwa katika 'quarters' haifikii uzito wa kg 50 kila pande. Ng'ombe wadogo kama hawa wanafaa kwa baadhi ya masoko ya ndani na kwa kusindikwa na kuwekwa kwenye makopo au kwa kutengeneza mazao ya nyama kama sausage.

Ng'ombe walionenepeshwa kwa molasses kama chakula cha msingi, huzalisha minofu mingi isiyo na mafuta mengi, mfugaji anaweza kupunguza matumizi ya molasses kwa kutumia chanzo chochote cha wanga, mahindi/ mtama kikichanganywa na urea. Unenepeshaji wa namna hii unafaa kwa ng'ombe wa kisasa ambao wanauwezo wa kukua kwa kiasi cha kg 1.5 hadi 2.0 kwa siku na kufikia uzito wa kg 400 baada ya miezi 12 hadi 14. Ng'ombe aliyenenepeshwa anauwezo wa kuzalisha nyama laini kiasi cha kg 250 inayouzika popote.

Utumiaji wa utaratibu huu ambao ni intensive Beef production utategemea uwiano wa gharama na soko.

Chanzo: <http://farmersmarket.co.tz>

Imepakuliwa: septemba 2021